UKOMBOZI NA WOKOVU

Ukombozi na Wokovu: Mpango wa masomo

Maelezo Mafupi

Somo la Kwanza:

I. Utangulizi.
II. Wokovu:
   A. Wazo kuu saba za kitheologia.
   B. Itikio la mtu kwa toleo ya wokovu.

Somo la Pili:

II. Wokovu: (inaendelea).
   C. Misingi ya wokovu.
III. Ukombozi.
   A. Utangulizi kwa wokovu.
   B. Adamu: Mwana historia hakika.

Somo la Tatu:

III. Ukombozi: (inaendelea)
   C. Adamu wa watu wote, wa kwanza na wa mwisho.
   D. Kristo kama mtu halisi.

Somo la nne:

III. Ukombozi: (inaendelea).
   E. Kristo bila zambi ya asili lakini akiwa na jaribu halisi.
   F. Utaratibu wa ukombozi: Kristo aliye fufuka analinganishwa na Adamu aliye anguka.
   G. Matokeo ya ukombozi: Kupata tena, kushinda, kupita zaidi.

Somo la Tano:

III. Ukombozi: (inaendelea).
   H. Ukuu wa Kristo juu ya Adamu.
   I. Kristo: Mkuu au Mjumbe wa taifa lililo kombolewa.
   J. Mwisho wa somo; Mtihani (mashindano).

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

Ukombozi na Wokovu: Mtihani (mashindano)

Maswali (maulizo) yanayoweza kukupatia alama 20

1) Hesabu na zieleze wazo kuu saba za kitheologia juu ya wokovu (uk. 195).

2) Tumia jina la kifupi "KUMAI" (kubali, maarifa na imani) kuelezea maana ya kuamini (uk. 198).

3) Onyesha ni jinsi gani Kristo anaweza akalinganishwe na Adamu ili kuelezea matengeneo za ukombozi (uk. 212, 213).

1) Chagua wazo kuu mbili za kitheologia juu ya wokovu na elezea ni jinsi gani zinahusiana na wokovu (uk. 195).

2) Kwa misemwa miwili (2) au mitatu (3) eleza ni kwa nini ni muhimu kushika maanani historia ya Adamu (uk. 202, 203).

3) Tumia maandiko mtakatifu mbili kutetea kanuni imani ya zambi ya asili (uk. 205).

4) Yesu alijifunzaje utii? Tumia andiko moja katika jibu lako (uk. 209).

5) Hesabu njia tatu maalum ambazo kwazo Adamu wa pili anaichukua nafasi ya Adamu wa kwanza kwa kutelekeza niaza Mungu kwa mwanadamu (haina haja ya rejeo zozote za maandiko; uk. 215, 216).

6) Onyesha njia moja ambazo sisi tuna zaidi katika Adamu wa Pili kuliko tulivyokuwa navyo katika Adamu wa kwanza (uk. 217).

UKOMBOZI NA WOKOVU

I. Somo la utangulizi.

Maelezo Mafupi

Mfano wa mwandishi:

Hadisi ya ukombozi na wokovu. Kijana mmoja alikuwa anapenda kuchezacheza ufukoni. Aliipenda sana mitumbwi. Kila siku alikaa mchangani akiangalia mitumbwi inayokuja na inayokwenda. Siku moja aliamua kujiundia mtumbwi wake mwenyewe. Kazi hii ilimchukua siku sita. Akamaliza kujiundia huo mtumbwi. Hakuweza kungojea kuuweka majini. Alipokuwa anauweka majini, mara moja upepo yakabadilika. Yakaukokota mtumbwi baharini, ukatokomea usionekane tena. Kijana alilia sanna kwa kuupoteza mtumbwi aliouunda mwenyewe na kuupenda sana. Kila siku alirudi hapo kwa matumaini ya kuupata mtumbwi huo ukiwa umetupwa ufukoni na upepo. Hakufanikiwa siku moja alipokuwa anatembeatembea kwenye mtaa wa maduka humo mjini, aliuona mtumbwi wake kwenye dirisha la maonyesho ya kuka. Ulikuwa ni ule mtumbwi wake uliopotea baharini. Mbio, akaingia dukani na kumwelezea mwenye duka kwamba huo mtumbwi hapo dirishani ulikuwa ni wake. Kama kawaida ya mfanya biashara, yule mwenyewe duka akamwambia kwamba mtumbwi huo utakuwa ni wake iwapo atalipa bei ya mtumbwi huo ambayo ni dolla 10. Kijana alibisha sana na kukazania kwamba mtumbwi huo ni wake, aliutengeneza yeye, hivyo hana haja ya kutoa hiyo doll 10. Hakufanikiwa. Hatimaye alilipa hizo dolla 10, feza pekee aliyo kuwa nayo. Kijana alipotoka nje, huku akiwa ameukumbatia mtumbwi wake alisema: **Ewe mtumbwi mdogo, wewe ni mali yangu mara mbili sasa wewe ni wangu kwa sababu nilikutengeneza, na sasa wewe ni wangu kwa sababu nimekununua.**
Mungu alituumba sisi. Halafu akalipa gharama (bei) kubwa sana kutukomboa. Hii ndiyo hadisi ya ukombozi na wokovu.

Tia Ufafanuzi wako:

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

A. Moyo wa Ukristo.

1. Kuanzia siku ile Adamu alipoanguka zambini katika bustani. Ya Edeni, Mungu amekuwa na mpango mmoja juu ya wanadamu. Mpango huu unaitwa ni mpango wa ukombozi na wokovu.

   a. Mpango huu unaweza kufuatiliwa kuanzia Mwanzo 3:15 hadi Ufunuo 22:14.

   b. Mpango huu ni mfungamano unaoishikilia Biblia pamoja. Ni muundo ambao ni msingi wa theologia yote.

   c. Biblia nzima inazungumzia ukombozi na wokovu.

2. Lengo la mwisho kabisa la Mungu kwa mtu ni wokovu. Watu wote wanaihitaji kuokolewa. Mungu anataka watu wote waokolewe (1 Timotheo 2:4; 2 Petro 3:9). Imani ya wokovu ndiyo "chimbuko" la theologia.

3. Ukombozi ni mpango wa wokovu. Hii ni matengenezo ya Mungu katika ukombozi.

B. Yaliyomo katika somo hii.

1. Kwanza, tutatoa uchunguzi wa jumla wa wokovu, uchunguzi huu utakuwa ni kwa kifupi sana, na utasaidia kututayarisha kwa uchunguzi maalum wa ukombozi.

2. Pili, tutauchunguza ukombozi kwa upande wa Kristo kama Adamu wa Pili, kwa uchunguzi huu tutaelewa zaidi ni nini kilichomo katika ukombozi, kwa nini unahitajika, na jinsi unavyotimilizwa.

UKOMBOZI NA WOKOVU

II. Wokovu - Kuokolewa.

Maelezo Mafupi

A. Wazo kuu saba za Kitheologia.

Fafanusi la mwandishi:

Kwanza tutafikiria upana wa wazo ya wokovu kwa kuhesabu wazo kuu saba za kitheologia ambazo zimo katika kanuni ya wokovu.

1. Ukombozi - Mpango ao matengenezo ya wokovu.
2. Wokovu (kuzaliwa mara ya pili kwa jinsi ya roho) - Ni hali halisi na nguvu ya kuokolewa.
3. Kufanya amani - Ni hali ya uhusiano ya wokovu.
4. Malipo (upatanisho wa Yesu Kristo kwa kufa kwake) - Ni kazi au gharama ya wokovu.
5. Kuhesabiwa haki - Ni matokeo ya kisheria, ya wokovu.
6. Uadilifu (haki) - Ni nafasi ya wokovu.
7. Utakaso (utakatifu) - Ni njia ya wokovu.

Kusudi ya mabishano

Tumia kielelezo ufuatao kuendeleza mabishano na kuzielewa zaidi wazo hizi saba ambazo zimo katika wokovu.

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

Wazo ya ukombozi	Tafsiri (fafanusi)	Maandiko matakatifu	Inafikiwaje	Itikio la mtu	Matokeo
Ukombozi	Kukirudisha hicho kilichokuwa kimepotea	Tito 2:14 Zaburi 103:4 I Petro 1:18 Wagalatia 3:13	Kristo kama Bingwa au Mshindi (1 Wakor. 15:57)	Imani: kuamini katika Mungu atawalaye na aliyeshinda	Heri, baraka Mamlaka Mafanikio
Wokovu	Kurudishia uhai, kuwekea maisha mapya uzimaupya kuzaa tena	Yohana 3:3-6 Waefeso 2:1 2 Wakor. 5:17 1 Yohana 5:1 Warumi 6:4-11	Kristo kama mpa uzima (Yohana 10:28; 1 Wakor.15:45)	Imani: kuamini kwamba Mungu anaweza na hutupa uzima mpya	Upya; Mabadiliko; Mwanzo mpya
Kufanya amani (upatanisho)	Kuleta mapatano kati ya maadui	2 Wakor. 5:19 Warumi 5:6-11 1 Yohana 1:3	Kristo kama mpatanishi (Waebrania 12:24)	Imani: kuamini kwamba Mungu anatupokea kama tulivyo	Ushirika; Undugu; Uhusiano na Mungu
Malipo (upatanisho wa Yesu kwa kufa kwake)	Kupatanisha mkosefu na Mungu kwa toleo takatifu	Warumi 4:6-9 1 Petro 1:19 Waebr. 9:13-22 2 Wakor. 5:21 Warumi 4:7	Kristo kama aliye badala yetu au toleo (1 Petro 3:18)	Imani: kuamini kwamba zambi zetu zinashugulikiwa Tubu: katika shukrani	Kuondolewa kwa uovu; msamaha
Kuhesabiwa haki	Kuhesabia mkosefu kama vile mwenye haki mbele ya Mungu	Warumi 5:1,9 Waebrania 5:9	Kristo kama asiye na zambi (2 Wakorintho 5:21)	Tubu: zambi zetu zinakuwa wazi (bila shaka)	Amani; Kuondolewa kwa hasira (ghadhabu)
Uadilifu	Kuwa safi mbele ya Mungu	Wafilipi 3:9 Warum 10:1-10 Waefeso 2:10	Kristo kama mjumbe wetu (1 Yohana 2:1)	Tubu: huku tukitambua kwamba hatuwezi kupata	Uhodari; Uhusiano na utakatifu
Utakatifu	Kutakasa na kutenga kando	1 Wathes. 5:23 Wafilip 2:12,13 Warumi 8:29 Waebrania 2:11	Kristo kama mfano wetu au mkamilishaji (Yohana 13:15; Waebrania 12:2	Tubu: Utaratibu unaoendelea wa kuigeukia zambi	Kubadilishwa na kuwa kama Yesu: Kazi njema.

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

Fafanusi la mwandishi:

Matokeo ya kila hali ya ukombozi yamejengwa juu ya msingi wa kuelewa kwamba Yesu yu ndani yetu sisi waamini (Wabalatia 2:20).

Itikio la mtu na hali ya ukombozi ni pamoja na hali mbili:
1) Tubu ao toba.
2) Amini (Marko 1:15).

Katika kielelezo tumechagua wazo moja au nyingine kwa kila moja ya "wazo" saba yenyi kuelezea ukombozi. Hata hivyo ni bora ikumbukwe kwamba kila wazo ina maitikio yote mawili.

B. Itikio la Mtu kwa tolea ya Wokovu.

1. Tubu.

   a. Maana au tafsiri yake: **Kugeuka** toka mambo ya kale kwenda kwenye mapya au toka kwa mabaya hadi kwa mema (Matendo 3:19).

      1) Hii si kule kujulia makosa tu (sikitikia).

      2) Hii si kule kujisikia vibaya tu (majuto).

   b. Kusudi (msukumo): Kwa nini utubu?

      1) Kwa sababu ya ukaribu na kuwepo kwake Mungu (Math. 3:2).

      2) Kwa sababu ya ujumbe wa injili (uzima, kifo, na kufufuka kwa Yesu).

         a) Uzito wa lile alilonifanyia Mungu ukilinganisha na hicho ninachostahili (Warumi 2:4).

         b) Uzito wa kile ambacho ni lazima nimtendee Mungu ukilinganisha na hicho Mungu anachostahili (Warumu 2:4).

Maelezo Mafupi

3) Kwa sababu ninahitaji ondoleo la dhambi zangu (Matendo 2:38; 3:19).

2. Amini (Imani).

a. Maarifa.

1) Ni muhimu (Warumi 10:17).

2) Hata hivyo, hayatoshi kuyafikia wokovu (Yakobo 2:19).

b) Kubali.

1) Kutambua na kukiri, kukubali ukweli wa injili. Ili lina maana kwamba kutakuwa na utii.

2) Kutambua na kukubali haja ya kazi ya Kristo inayookoa. Hili lina maana kwamba kuna kutegemea.

c) Tumaini (Imani).

1) Mtu anajigeukia mwenyewe (Mithali 3:5, 6).

2) Anamuangilia Kriso (Waebrania 12:2).

3) Nukta hizi zina maana kwamba kuna uhusiano binafsi.

Fafanusi la mwandishi:

Ili kuweza kuzikumbuka hali hizi tatu za "imani" unaweza ukatunga jina kwa ufupi kwa kuchukua herufi za mwanzo za Kubali (Ku) Maarifa (Ma) na Imani (I) - KUMAI
Kumbuka: Ili kuamini inabidi kumai kwa sababu imani ya kweli maana yake ni utii (Yakobo 2:17).

3. Kujisalimisha.

   a. Sehemu ya mtu katika utaratibu wa ukombozi ni kupokea (Yohana 1:12). Ili kuweza kupokea ni lazima mtu atubu na kuamini. Ili aweze kutubu na kuamini ni lazima ajisalimishe.

   b. Inabidi aache kupigana na Mungu (Kushindana na Mungu). Kutubu kwenyewe hasa na imani ni kitendo cha kujisalimisha (Mathayo 16:24, 25).

C. Misingi ya Ukombozi.

1. Kuna vitu vinne (4) ambayo sharti Mungu avifanye katika ukombozi.

   a. Kumvutia mtu kwake (Yohana 6:44).

   b. Amtie uzima upya mtu huyo (Yohana 3:1-5).

      1) Yoani ni lazima mtu azaliwe toka juu.

      2) Angalia jinsi Yesu alivyozaliwa toka juu (Luka 1:35).

   c. Safisha dhambi (Yohana 13:5-10; Matendo 22:16).

      1) Hili linawakilishwa na ubatizo kwa maji.

      2) Angalia jinsi Yesu alivyobatizwa (Marko 1:9).

   d. Mpe mtu nguvu za kuishi maisha ya kikristo (Matendo 1:8; 2:38).

      1) Hili linafanywa katika ubatizo wa roho Mtakatifu.

      2) Angalia jinsi Yesu alivyobatizwa katika roho Mtakatifu (Marko 1:10).

2. Kazi ya msalaba na njia ya **Wokovu.**

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

Kusudi ya mabishano

Chungua kielelezo unaofuata na andalia mabishano ya kutengeneza jambo.



a. Kazi ya Msalaba (A hadi D).

1) Hii inajumulisha yale ambayo Yesu ilibidi anifanyie. Hii si pamoja na kazi zangu mwenyewe.

2) Lengo ni kwenye imani katika Kristo.

3) Angalia jinsi ukombozi kwa wana "theologia ya kazi" itabidi uhakikishe kwamba mfu anaweza kupanda kilima kati ya mtu aliyeanguka na mtu aliyeokolewa.

b. Njia ya Msalaba (E hadi Z).

1) Hii inafunzwa kwa baada ya wakatina na ukomavu.

2) Hasa hasa inajumulisha kujifunza kujitia nira ya Yesu na kujifunza kumruhusu Yesu kuishi ndani yako (Mathayo 11:29; Wagalatia 2:20).

Kusudi ya mabishano

Yupi tofauti kuu katikati ya kazi ya msalaba na njia ya msalaba? Jinsi gani tofauti hii inatenga dini ya kikristo kati ya madini nyingine zote na elimu ya kidunia?

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

III. Ukombozi.

A. Utangulizi kwa Ukombozi.

1. Tafsiri (fafanusi).

   a. Kama tulivyokwisha kutambua hapo awali, ukombozi ni mpango au matengenezo ya wokovu.

   b. Ni hatua na utaratibu wa kurudisha hicho kilichokua kimepotea.

      1) Kukomboa ni kukipata tena.

      2) Ni kukirudisha au kukidai hile ambacho kwa asili ni chako.

2. Toka kwa Adamu wa kwanza hadi Adamu wa mwisho (toka kifo hadi uzima).

   a. Karibu vitu vyote ambavyo pale mwanzo Mungu alimpa Adamu, vilipotea alipoanguka. Ilitakiwa vikombolewe. Yesu Kristo, Adamu wa Pili (1 Wakorintho 15:45) alikuja kukikomboa kile ambacho Adamu wa kwanza alikuwa amekipoteza.

      1) Biblia inaifuatilia hadisi hii ya ukombozi kwanzia kwenye maisha ya Adamu wa kwanza hadi kwenye maisha ya Adamu wa Pili.

      2) Yaani, inafuatilia hadisi ya ukombozi toka kifo hadi uzima, au toka hicho kilichopotea hadi hicho kilichokombolewa.

   b. Paulo anarejea kwenye hali hii ya ukombozi katika 1 Wakorintho 15:20-26 na Warumi 5:12-21 anapojenga kile tunachoweza kukiita theologia ya Adamu-Kristo.

      1) Sehemu nyingine yote ya somo hii itatenga kwenye theologia hiyo tunapochungua wazo ya ukombozi.

      2) Majifunzo yetu itajali maneno yafuatayo, ambayo hayajathibitishwa:

Maelezo Mafupi

a) Ili Yesu aweze kustahilishwa, bila ya kupigwa, kuwa ni masiya, itabidi arudishe (komboa) kwa watu hali ile ya utu ambayo Adamu aliipoteza alipomuasi Mungu.

b) Yesu ndiye aliyekuwa ni utimilifu wa nia ambayo pale mwanzo Mungu alikuwa nayo kwa ajili ya mwanadamu. Uhusiano kati ya Adamu wa kwanza na Adamu wa Pili ni sawa na uhusiano kati ya mwanadamu aliyeanguka na mwanadamu aliyekombolewa.

Kusudi ya mabishano

Kumbuka hadisi ya "ahali mkombozi" katika kitabu cha Ruthu (2:20; 3:2; 3:9-13; na 4:1-22).

Angalia jinsi hii ni mfano (au kuonyeshwa kwa fumbo) ya Kristo, huyu aliyebidi kuja nyuma kama "ahali mkombozi" wa ulimwengu. Kwa kifupi, zungumzeni juu ya mifano nyingine yenyi kuelekea hii hali ya elimu ya nguvu zinazoendesha na kuonyeshwa kwa fumbo ujio wa Kristo katika agano la kale. Vielelezo hivi vya agano ya kale vina maana gani kwa kufunua ujio wa Yesu?

B. Adamu: Mtu Kweli wa Kihistoria.

1. Katika masingira mengi ya kiinjili, si suala la muhimu sana kuitetea hali ya kihistoria ya Adamu. Biblia inakubaliwa kwa uhakika kabisa kuwa ni neno la Mungu.

2. Walakini, katika vikundi vingine vya watu wa madini, ipo sura nyingine ya hadisi ya Adamu na Eva ambayo haiwafikirii Adamu na Eva kuwa hasa watu wa kihistoria.

   a. Badala ya kuikubali hadisi kama masimulizi ya kihistoria, inatafasiriwa kama ni kisa chenye maana iliyofichwa fumbo.

   b. Inasema kwamba hadisi hii ni "mfano tu wa kufundishia."

3. Walakini, atari za kitheologia za kumkataa Adamu wa kihistoria inaleta matatizo makubwa.

   a. Kama Adamu wa kwanza hakuwa halisi, ni kwa nini basi tumemuhitaji (tunamtaka) Adamu wa Pili? Matokeo ya mwisho ya kufuata fikira za aina hii, yako wazi:

Maelezo Mafupi

1) Uhistoria wa Yesu mara nao unakuwa wa mashaka.

2) Halafu miujiza ya Yesu inakuwa ya mashaka.

3) Mwisho, Umungu wa Yesu unakuwa wa mashaka.

b. Wale wanaoshauri "mfano wa kufundishia" hawauoni utenganisho kati ya dhambi na kuumbwa. Zambi na kuumbwa vinaangaliwa kama vile vinakaa pamoja.

1) Hivyo, dhambi inaonekana kama ni sehemu ya asili ya mwanadamu na kuumbwa. Yaani ni ya mtu kwa asili yake.

2) Kama hivyo ndivyo, basi Yesu hawezi kumwakilisha mtu wa asili.

3) Na zaidi ya hapo, inazaifusha wazo la binadamu la kuwa na hofu ya zambi.

4) Kutokuwa na hofu kunaleta upungufu wa nia ya kutubu ambayo inasababisha upungufu wa kuungama ambako kunaleta upungufu wa msamaha wa dhambi.

5) Haya yote, tena yanaleta upungufu wa haja ya Yesu wa kihistoria na ukombozi ambao anatoa.

Kusudi ya mabishano

Uonaje! Jinsi, kumkana Adamu halisi wa kihistoria huharibu kazi ya mwokozi halisi wa kihistoria? Zungumzeni juu ya maulizo au fafanusi nyingine.

C. Adamu wa Watu Wote, wa Kwanza na wa Mwisho.

1. Pamoja na kumwangalia Adamu kama mtu halisi wa kihistoria, ni lazima pia aangaliwe, kama Adamu wa ulimwengu anawakilisha mtu.

a. Kwa kweli, neno la kiebrania linalotumika kama Adamu lina maana ya "mtu."

b. Hivyo mapatano ya ki-Adamu yalikuwa ni mapatano na mtu. Mapatano yalipovunjwa, yalivunjwa na mtu.

Maelezo Mafupi

1) Tunapoelewa kwamba Mungu alifanya mapatano na mtu, na mtu akayavunja mapatano hayo, basi tunaelewa kwamba tunahitaji upatanisho wa watu wote.

2) Yesu, kama Adamu wa Pili, alikufa kwa ajili ya watu wote. Alikufa kwa ajili ya Myahudi na mtu wa mataifa (angalia kwamba Paulo hamwiti Yesu Musa wa Pili).

3) Yesu alikufa kwa ajili ya watu wote kwa sababu watu wote wana hofu kwa kuyavunja mapatano. Alikufa kwa ajili ya watu wote kwa sababu wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu (Warumi 3:23).

2. Kama jinsi Luka alivyo mwangalifu katika kuuelezea ukuu wa Yesu hadi kwa adamu (Luka 3:38), vivyo hivyo Paulo ni mwangalifu pia kumtambua Adamu na zambi yake kama inahusika katika mpango wa ukombozi.

   a. Sura la pili (2) la waefeso imejaa theologia ya Paulo juu ya ukombozi.

   b. Soma na jifunza Waefeso 2:1-3, 11, 12.

      1) Paulo anaelezea haja ya watu wa mataifa kukombolewa (mstari wa 11, 12).

      2) Pia anakuwa mwangalifu sana katika kuielezea haja ya wayaudi kukombolewa (mstari wa 3).

         a) Paulo analeta kuelewa kwamba kuna haja ya kuwa na nia ya pamoja ya kuwepo kwa jawabu la pamoja.

         b) Katika theologia yake basi, anaeleza jinsi Adamu alivyokuwa ni mwanzilishi wa haja hiyo ya pamoja yaani, kuanguka kwa mtu (asili ya dhambi) kunahitaji ukombozi.

3. Kwa Myahudi, Adamu alipotenda dhambi, wote walitenda dhambi katika yeye. Yaani, kuanzia hapo mtu angelikuwa na dhambi ya asili.

   a. Kama vile mwimba zaburi anavyosema, tumezaliwa katika dhambi (Zaburi 51:5).

Maelezo Mafupi

b. Kama vile Paulo anavyosema, tuna dhambi ya asili (Waefeso 2:3).

c. Anaielezea zaidi kanuni na imani ya zambi ya asili katika Warumi 5:12,16. Tena basi, ukombozi wa wote (ukombozi kwa Myahudi na mtu wa mataifa) kitheologia, ni muhimu sana kwa sababu dhambi ya wote, na kifo, kitheologia ni halisi.

Kusudi ya mabishano

Zungumzeni juu ya maulizo au fafanusi nyingine zenyi kuelekea uasili ya dhambi ya Adamu kwa watu wote na uasili ya ukombozi kwa wote katika Kristo.

D. Kristo kama mtu Halisi.

1. Je, dhambi kwa wote, na kifo, vilikuwa ni sehemu ya mpango wa Mungu kwa mtu? (angalia Warumi 1:18-25).

   a. Ni wazi aya hizi zimeshawishika na yaliyomo katika mwanzo.

      1) Kwa asili, mtu aliumbwa ili amtumikie muumba.

      2) Baada ya kutumikia, hiki kiumbe mtu, kinakuwa kitu kidogo kuliko kilivyokuwa hapo mwanzo.

   b. Chungua Warumi 1:23.

      1) Ni nini maana halisi za neno "wakaubadili"?

      2) Ni nini maana halisi za tofauti kati ya "asiye na uharibifu" na "aliye na uharibifu."

   c. Tunaweza tukasema kwamba Adamu kwa asili yake alikuwa na hali ya kuweza kuishi milele.

      1) Kweli, mti wa uzima ulikuwa bustanini na ulikuwa ni mmoja wa mti ambayo Adamu angeliweza kutumia (Mwanzo 2:9,16).

Maelezo Mafupi

2) Kama Adamu kweli hakuwa hata na hali ya kuishi milele, basi kuipoteza hali hiyo isingelikuwa hasa ni dhambi. Lakini Mungu anautumia uwezekano wa kifo kama adabu hakika (angalia Mwanzo 2:17).

2. Adamu wa asili angeliweza kuwa kitu kingine zaidi ya hivyo ambayo alikuwa. Maana halisi ya wazo la ukombozi ni kwamba Adamu wa pili akawa kama Adamu wa kwanza alitakiwa kuwa. Adamu wa pili alipata ushindi nafasi yale Adamu wa kwanza alianguka.

   a. Yesu Kristo, mpatanishi kamili akawa "matunda ya kwanza" (fikiria 1 Wakorintho 15:20) - (matunda ya kwanza, katika masemi ya wakulima ni mauwa ya kwanza ya upya yenyi kuota baada ya kupanda mbegu. Hiyo ni alama na ahadi ya furaha kwamba ukomavu wa mimea na matunda itafuata.

   b. Fikiri maneno yafuatayo: Si utu wa Adamu ndio asili, Bali wa Kristo.

      1) Katika sura tukufu ya Mungu, utu wa Kristo unatangulia utu wa Adamu katika hali kwamba nia ya Mungu kwa mtu inatangulia uasi wa Adamu.

         a) Adamu, ambaye anaelekea ni wa kwanza, kwa kweli ni wa pili.

         b) Kristo, ambaye anaelekea ni wa pili, kwa kweli ni wa kwanza.

      2) Wataalamu wengi wanatetea kwamba Adamu ni bora itafsiriwe kuwa "mtu au mtu huyu." Kwa bahati mbaya, akawa "si mtu wa asili."

      3) Katika Yohana 19:5: Pilato anatangaza: "Tazama, mtu huyu." Kwa bahati nzuri, Yesu ni "mtu asili." Kwa kuwa Adamu wa kwanza ameshindwa (ameanguka), Kristo, ni huyu Adamu wa pili aliyetimiza mapenzi yote ya Mungu (Isaya 53:11,12).

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

3. Ni muhimu kuelewa kwamba hali ya maisha ya awali na yaliyotarajiwa, ya Adamu (mtu) imetimizwa katika maisha ya Yesu.

   a. Kuelewa huku kutatusaidia sana sisi kuitambua gharama kubwa ambayo Yesu alilipa hapo msalabani.

      1) Katika nafasi yake kama Adamu wa pili, Yesu alikuwa na uwezo wa kuishi milele. Dhambi ndiyo huleta kifo (Warumi 6:23), na Kristo hakuwa na dhambi (Waebrania 4:15). Hakuwa na haja ya kufa.

      2) Alikufa bila ya kulazimishwa.

      3) Tunaweza kusikia maana halisi za kifo hiki cha kuchagua.

         a) Maana halisi za upendo kubwa wa Mungu kwa kuumba kwake.

         b) Maana halisi za upatanisho na wazo ya Kristo kama ni wa badala yetu.

   b. Kuelewa huku pia kunatusaidia sisi kutambua jinsi kuumba na enzi ni mpango katika ukombozi.

Fafanusi ya mwandishi:

Yesu, kama vile Adamu halisi alitimiza hata zaidi, mahitaji yote ya walimwengu. Hatimaye alitimiza mahitaji yote ya kimungu. Alikuwa Mtu, pia Mungu kamili. Katika ummoja lakini katika nafsi mbili. Hii ndiyo siri au fumbo inayosherekewa katika kanisa la Kikristo. Na papo hapo ni mwanzo wa kunuliwa kwa madini mengi za uwongo. Hakuna dini ingine inayokubali fumbo ya utu na Umungu wa Yesu.

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

1) Yesu alizaliwa bila dhambi ya asili. Alizaliwa kama Adamu wa asili. Hakuzaliwa akiwa na dhambi ya asili. Hakuzaliwa kama Adamu mwingine.

   a) Hivyo, anaitimiza asili ya mtu na sio kuiteketeza.

   b) Na hivyo, katika Warumi 8:3 Paulo anasema kwamba alitumwa "katika mfano" wa mwili ulio na dhambi.

   c) Alitumwa katika "mfano" ("omoi" katika lugha ya kigriki) sio "kama" ("omo" katika kigriki). Tofauti moja katika lugha ya kigriki ni nukta kidogo tu.

2) Maana ya haya yote ni kwamba uumbaji na ukuu wa ukombozi hauteketezi hali ambayo mtu alikuwa, bali inatimiliza hali ambayo mtu anatakiwa awe.

   a) Ukombozi hurudisha hicho ambacho mtu alipoteza, hicho ambacho mtu amekifanya, haukigeuzi.

   b) Ukombozi ni hasa ongezo na wala si kitendo cha kupunguza unaongeza hicho ambacho hapo awali kingelikuwepo bila ya kutoa (mpaka Bwana arudipo na kuumba upya mbingu na nchi) kile kilichokuja baadaye).

      (1) Hivyo, mtu aliyekombolewa bado anaweza akawa anaishi katika ulimwengu ulioanguka.

      (2) Tunaweza kuuona ukombozi katika maisha yetu wakati tukiendelea kupambana na matokeo ya matendo yetu ya zamani.

      (3) Ilibidi Paulo azungumzie juu ya uhalali wa hali hizi mbili (angalia Wagalatia 5:17 na Warumi 7:14-20).

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

E. Kristo Bila Zambi ya Asili Lakini Akiwa na Jaribu Halisi.

1. Yesu hakuwa "sawa sawa" ya mwili wenye zambi kwa sababu hakuzaliwa kwa mtu bali kwa Roho Mtakatifu.

2 Yeye kama Adamu, alizaliwa bila kuwa na dhambi ya asili.

3. Adamu hawa wawili walikuwa ndio watu pekee ambao walikuwa na uwezekano wa kuishi maisha kamilifu.

   a. Aliposhindwa Adamu, Yesu alifanikiwa.

   b. Hii ni njia moja kuelezea ni nini hasa kilitokea ili ukombozi uwe ni halisi.

4. Hata hivyo, yeye (Yesu) kama Adamu, alijaribiwa.

   a. Majaribu haya ni halisi kabisa Yesu hayapishi tu hivi hivi, anashindana nayo.

      1) Kufuatana na Waebrania 5:7,8 - Yesu aliteswa ili kujifunza utii. Aliteseka vipi? Aliteseka kupitia majaribu ya mwili wake (mstari wa 7).

      2) Kuna thamani katika ukombozi. Thamani haikulipwa tu msalabani, bali ililipwa katika maisha yote ya Yesu alipokuwa anajiandaa kuukabili msalaba.

      3) Alijifunza utii (aliyashinda majaribu) kwa kupitia vitu ambavyo vilimtesa.

      4) Katika siku zake za mwili (katika siku za majaribu yake) alitoa maombi kwa kilio na machozi.

         a) Kudai kitu asili wakati huteketezi kabisa hicho ambacho si cha asili, inasababisha mateso. Kweli kabisa hii inafanyika pia kwetu wakati Mungu anafanyiza ukombozi wake.

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

Kusudi ya mabishano

Ipitie tena hoja hii kama jinsi inavyohusiana na mabishano wa hapo juu unaohusu ukombozi kama ongezo, kama ni tofauti na kutoa. Sasa fikiria jinsi haya yote yanavyotuhusu sisi. Ni nini maana halisi zake?

b) Ili kukusaidia kulijibu swali (ulizo) hili, fikiria uhakika wa 2 Timotheo 3:12. Inabidi tukumbuke kwamba katika ukombozi wetu tunafanywa jamii mgeni (ulimwengu huu si makao yetu) sisi ni viumbe wapya (ambao bado wanapambana juu ya kushindana na viumbe vya zamani vilivyo ndani yao) tukiishi katika ulimwengu uliojaa viumbe vya zamani ni vitu asili kupambana na vile visivyo vya asili. Vile halisi hushindana na vile vya kutunga. Kama ilivyo na Yesu hili linasababisha mateso (Yohana 15:20).

c) Hivyo, kwa hali fulani (katika hali kama ilivyo katika Wagalatia 2:20 ni kweli), mateso ya kukomboa yanaendelea kwa sababu mapambano ya yaliyo ya asili kushindana na yale yasiyo ya asili yanaendelea (Wakolosai 1:24; Wagalatia 6:17).

b. Majaribu yalikuwa halisi kwa Yesu kwamba Biblia inatuambia kwamba Yesu anaweza kuona Huruma kwa jinsi tulivyo wadhaifu (Waebrania 4:15).

c. Majaribu yanaweza yakawekwa katika mafungu matatu (jifunze 1 Yohana 2:16).

1) Tamaa ya mwili.

2) Tamaa ya macho.

3) Kiburi cha uzima.

a) Eva aliyapitia yote haya alipokuwa bustanini (Mwanzo 3:6)

(1) Tamaa ya mwili: "Mti wafaa kwa chakula."

(2) Tamaa ya macho: "Wapendeza macho."

(3) Kiburi cha uzima: "Mti wa kutamanika kwa maarifa."

b) Yesu aliyapitia yote haya huko jangwani (Mathayo 4:1-11).

(1) Tamaa ya mwili: "Amuru kwamba mawe haya yawe mkate" (mstari wa 3).

(2) Tamaa ya macho: "Akamwonyesha ufalme zote za ulimwengu na utukufu yake" (mustari wa 8).

(3) Kiburi cha uzima: "Jitupe chini" (kuonyesha jinsi ulivyo maalum: mstari wa 6).

Fafanusi la mwandishi:

Ni bora iangaliwe kwamba Luka (4:1-13) anaubadili mpangilio wa majaribu ukilinganisha na Mathayo. Badiliko hili linaufanya mpangilio wa majaribu ya Yesu sawasawa na mpangilio wa majaribu katika 1 Yohana 2:16 na mwanzo 3:6.

Lakini hili lisitushangaze. Injili ya Luka pia ni tofauti na injili ya Mathayo. Ukoo wa Yesu katika Luka unakwenda nyuma hadi kwa Adamu ambayo Mathayo yeye anakwenda nyuma hadi kwa Ibrahimu.

Kumbuka kwamba injili ya Luka ni "kwa watu wote." Inalenga watu wote. Inasisitizia ukombozi kwa watu wote. Inasisitizia ukweli kwamba Adamu wa pili, ili kumkomboa mwanadamu, ilibidi ayapitie majaribu yale yale kama ya Adamu wa kwanza. Hakika, hii ni sehemu muhimu sana ya ukombozi.

d. Mpaka hapo Yesu alipoyashinda majaribu ya mwisho ya maisha yake (fikiria mapambano katika Luka 22:44). Utakatifu wake ulikuwa ni utakatifu ambao Adamu aliokuwa nao kabla ya kuanguka.

e. Habari njema, na zitakuwa hivyo milele. Yesu Kristo alikuwa mshindi juu ya majaribu haya.

1) Utakatifu wa Kristo usio halisi ukawa utakatifu halisi na kamili. Hatua hii ya jaribu kuu ilikuwa ni ya lazima ili kuweza kuufanya ukombozi uwezekane.

2) Na hivyo, Kristo aliutimiliza kwa ustahili wake mwenyewe ushindi wake juu ya majaribu ulikuja kwa kupitia mateso na ukasababisha utii kamilifu.

Kusudi la mabishano

Inatupasha tutie theologia yetu katika matendo. Kama vile viongozi wa kanisa, majaribu gani inayowatukia zaidi? Je! Unajisikia nguvu kwa kutambua kwamba Yesu alipata ushindi juu ya majaribu ya aina hayo? Je! Unaweza kufikiliza kwamba, Kristo ndani mwetu, sisi pia tunaweza kupata ushindi? Chukueni muda wa kuombeana ili mupate ushindi juu ya matokeo hizi.

F. Matengeneo ya Ukombozi: Kristo Aliye Fufuka Analinganishwa na Adamu Aliyeanguka.

1. Kutotii kuhilinganishwa na kutii.

a. Jifunza Warumi 5:19.

1) Adamu wa kwanza alianguka. Hakuwa mtiifu.

2) Adamu wa pili alinyenyuka alikuwa mtiifu.

b. Kumbuka, utiifu hii Yesu alijifunza, na ilihakikishwa katika majaribu.

1) Umungu wake haikuwa kisingizio cha kumzuia katika utu wake kupambana na mambo mbali mbali yanayotukia wanadamu.

2) Ilikuwa kitendo kiadilifu kilichokua kutokana na asili yake ya utu.

c. Pitia tena Waebrania 5:8.

1) Ukombozi unahusika sana na upande wa utu wa Kristo.

2) Umo katika msingi wa utii wa kujifunza ambao ulikuja kupitia mateso ambayo mwandishi wa Waebrania anasema: "Naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii."

2. Kiburi kililinganishwa na unyenyekevu.

a. Jifunza Mwanzo 3:5 na Wafilipi 2:6.

1) Adamu wa kwanza alianguka, alitaka awe kama Mungu Adamu ni mtu aliyetaka kujiweka mwenyewe awe kama Mungu.

2) Adamu wa pili alinyenyuka. Hakuwazia hata kidogo usawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho.

3) Yesu ni Mungu ambaye yuko tayari kujishusha mwenyewe ili awe kama mtu. Na tena, Mungu alitangaza upendo wake usio na mwisho na bei ya mtu kwa kujibadilisha hata mwenyewe katika Kristo sababu ya ukombozi wa mtu.

b. Ukombozi ulikuja wakati Kristo alikibadili kiburi kilichosababisha kuanguka kuwa unyenyekevu wa Mungu unaoleta utukufu.

Kusudi la mabishano (mazungumzo)

Kama ukombozi wetu ulikuja toka utii na unyenyekevu, je basi tunaruhusu kuto kutii na kiburi maishani mwetu? Mzungumzie suala hii na mpate kutoa njia bora ao majibu.

Maelezo Mafupi

G. Matokeo ya Ukombozi: Kupata Tena, Kushinda, Kupita Zaidi.

1. Kukipata hicho kilichokuwa kimepotezwa.

   a. Uhusiano na Mungu.

      1) Haja kubwa ya mwanadamu ni kumjua Mungu. Mtu alitakiwa kutafuta lengo na kusudi (shauri) katika maisha kwa kupitia uhusiano wake na Mungu.

      2) Lakini basi, Adamu alipotenda zambi, alijenga ukuta kati ya mtu na Mungu.

         a) Adamu wa kwanza alijenga ukuta. Adamu wa pili aliuvunja hata milele.

         b) Yesu humfunua Mungu kwa mwanadamu. Aliuvunja ukuta ambao Adamu alikuwa ameujenga. Sasa amesimama kama yule ambaye kwa kupitia kwake mtu anaweza kuwa na ushirika na Mungu.

         c) Katika hali ya ukombozi, Kristo akawa ndiye mpatanishi kamili ili kuipata kusudi (shauri) ya juu kabisa ya Mungu juu ya mwanadamu.

   b. Kupata tena utukufu wa mwanadamu.

      1) Utambulisho wa juu kabisa wa mwanadamu ni kwamba aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Hili ni pamoja na aina ya utukufu ambao mwanadamu alikuwa nao (2 Wakorintho 3:18 na Warumi 5:2).

      2) Adamu aliupoteza utukufu huo. Alinyanganywa kile.

      3) Jifunze Warumi 3:23.

         a) Usemi huu "kupungu kiwa" unaweza ukatafsiriwa kama "kushindwa kufika" au "kupoteza."

         b) Utukufu wa mwanadamu aliokuwa nao ulipotezwa wakati wa kuanguka.

c) Umepatikana tena katika Kristo wakati tunabadilishwa tufana ne na mfano huo huo toka utukufu hata utukufu (2 Wakorintho 3:18).

2. Kumshinda yule aliyekuwa ameshinda.

   a. Kwa sababu Adamu wa kwanza "alipoteza" utukufu wake kwa shetani humo bustanini, Adamu wa pili ilibidi amshinde shetani msalabani, aishinde kifo na dhambi, hivyo kumrudishia mtu nafasi ya utukufu wa milele, pia furaha ya Baba.

   b. Adamu wa pili anakuja kama yule anayeupata tena, na kama yule anayeshinda.

      1) Yesu alipomshinda shetani pale msalabani, aliishinda kifo, na kaburi. Alipata tena pale mahali kwa ajili ya mwanadamu. Juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo (Waefeso 1:21).

      2) Mwanadamu anashiriki katika mateka ya ushindi huu katika hali kwamba akafufuka pamoja naye. "Anatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa Roho" (Waefeso 2:6).

   c. Yesu, hapo msabani alimshinda shetani, alishinda kifo.

      1) Kifo hakikuwemo katika mpango asili wa Mungu juu ya mwanadamu (Mwanzo 2:17).

      2) Kwa ufufuo, Adamu wa pili alikishinda kifo (Warumi 6:9).

      3) Kwa Adamu wa Pili, kifo kikafutwa kabisa kwa wote (1 Wakorintho 15:26). Tumekombolewa toka kwenye kifo (Waebrania 2:14,15).

3. Kuirudisha hali awali kwa njia ya utimilizo. Adamu wa pili anakuwa ni badala ya Adamu wa kwanza kwa kuitimiliza kusudi ya Mungu kwa mwanadamu.

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

Kusudi la mabishano (mazungumzo)

Jifunze kielelezo ifuatayo na uendeleze mabishano au mazungumzo inayoelekea Adamu wa kwanza na wa pili.

KATIKA ADAMU WA KWANZA	KATIKA ADAMU WA PILI	MAANDIKO MATAKATIFU
Wengi walifanywa watenda dhambi	Wengi watafanywa wenye haki	Warumi 5:19
Tumehukumiwa kifo	Tuna uzima wa milele	Warumi 5:12,21 1 Wak. 15:26
Tunashirikishwa katika asili yake ya kuanguka	Tunakuwa viumbe wapya	Mwanzo 5:3 2 Wak 5:17
Tunafungwa na misukosuko bila hata kupumzika	Tuko huru katika raha ya milele tunayoipata ndani yake	Waebrania 4:1-3 Wagalatia 5:1
Tumelaaniwa kuhukumiwa	Tunapewa hakikisho ya uhaki na maisha	Warumi 6:18

H. Ukuu wa Kristo juu ya Adamu.

1. Ni kweli kwamba mwanadamu aliyekombolewa sasa ana asili mbili. Wanapambana wao kwa wao. Hata hivyo, ni vema kuona kwamba Paulo hawazungumzii hawa wawili katika hali ya usawa.

   a. Nguvu za matokeo ya matendo ya Adamu wa pili ni kuu kuliko nguvu za matokeo ya matendo ya Adamu wa kwanza.

   b. Nguvu za neema ni kubwa kuliko nguvu ya dhambi (Warumi 5:20).

   c. Uhusiano wa Adamu wa pili na Adamu wa kwanza ni ya kindugu (ya binadamu) uhusiano wa Adamu wa Pili na Adamu wa kwanza si halisi, unategemea Adamu wa Pili "ni zaidi" (Warumi 5:9, 10, 15, 17, 20).

Maelezo Mafupi

1) Katika Warumi 5:12-21 Paulo anatupa picha ya Kristo kama yule mmoja ambaye anamzidi yule mwingine (Adamu).

2) Ipo hali kwamba njia pekee ambayo hawa Adamu wawili wanahusiana ni kwa sababu huyu wa pili ni mkuu zaidi kuliko wa kwanza kwa hali zote.

3) Paulo hamlengi Adamu kuona ni jinsi gani anahusiana na Kristo - yeye Paulo analenga kwa Kristo kuona ni jinsi gani anahusika na Adamu.

2. Mungu humtafuta mwanadamu. Mwanadamu hamtafuti Mungu (Yohana 15:16; Luka 15:1-7; Warumi 10:6,7).

   a. Neema ya Mungu ni ya ushindi wa hali ya juu kabisa juu ya zambi ya mwanadamu.

   b. Kwa njia zote zile, tuna zaidi katika Adamu wa Pili kuliko katika Adamu wa kwanza.

Kusudi la mabishano (mazungumzo)

Tumia kielelezo ifuatayo kuielezea kwa mazungumzo namna sisi waamini tuna zaidi katika Kristo kuliko yenye tuliyokuwa nayo katika Adamu wa kwanza.

ADAMU WA KWANZA	ADAMU WA PILI	MAANDIKO MATAKATIFU
Aliumbwa kwa mfano wa Mungu, kulingana na sura ya Mungu	Anangaa kwa utukufu wake na uwakihishaji sahihi wa asili yake	Mwanzo 1:26 Waebrania 1:3
Alipokea uhai wake toka kwa Mungu ambaye alimpumulia puani pumzi ya uhai	Akawa Roho mtia uzima	Mwanzo 2:7 1 Wak. 15:45
Toka udongoni	Toka mbinguni	1 Wak. 15:47

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

I. Kristo: Mkuu au Mjumbe wa Taifa Lililokombolewa.

1. Kristo ni kichwa cha "mwanadamu mpya," wakati Adamu ni kichwa cha mwanadamu wa zamani.

   a. Tamshi hili ni bora lieleweke pamoja na kuelewa kwamba hakuna utu ulioanguka (Adamu) na utu "upya" kabisa ("Mpya" kwa maana kwamba hakikuepo kabisa tangu mwanzo).

   b. Kristo si Adamu mpya. Yeye ni Adamu wa pili. Yaani ni Adamu wa asili.

      1) Hivyo, tunazungumzia utu ulioanguka na utu uliokombolewa (uliorejeshwa kwenye hali yake ya mwanzo).

      2) Yesu si mwakilishi wa Taifa jipya kama alivyo mwakilishi wa utu kamilifu. Yeye ni Adam halisi, lakini zaidi katika ushindi. Huu ni ukombozi.

2. Imani katika utu inachanganyikiwa juu ya utu.

   a. Mtaalamu anapendezwa na utu na anaaminia uzuri (uwema) wa mtu bila haja ya ukombozi. Kusema kweli, anautamani utu ulioanguka, uliovunjika na unayepevushwa.

      1) Adamu wa kwanza ndiye Mungu wake.

      2) Kwa hivyo, anakufa na Adamu wa kwanza (Warumi 6:23).

   b. Mkristo anamwangalia adamu wa pili. Anatamani utu halisi imeumbwa upya kwa kudumu kwa roho wa uzima katika Kristo.

      1) Adamu wa pili ndiye Mungu wake.

      2) Kwa hivyo, ana fufuka na Yesu (1 Wakorintho 15:2, 20, 23).

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi

J. Mwisho wa somo.

1. Tunapozaliwa tunayapata yale ya Adamu wa kwanza. Kuokolewa ni kuzaliwa tena. Ni kuyapata yale ya Adamu wa pili. Kwa kuwa kuna kuzaliwa kwa aina mbili, tuna asili mbili zimo katika mapambano ya kudumu. Lakini tunaweza kushangilia katika ukuu wa Adamu wa pili juu ya Adamu wa kwanza, na kwa hiyo ukuu wa asili yetu "mpya" juu ya asili yetu ya "zamani."

2. Adamu alishindwa. Kristo alishinda. Kwa kiasi kwamba tunaruhusu asili mpya (Kristo) kuyatawala maisha yetu ni kiasi ambacho ndio utakuwa ni ushindi wetu pia. Hallelujah!

UKOMBOZI NA WOKOVU

Maelezo Mafupi